**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI TUNDURU …………

**RUVUMA-TUNDURU**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**Namba za Simu**

**Mkuu wa Shule 0787927992/0628160051**

**Makamu Mkuu wa Shule 0755703438/0689214583**
**Patron 0765222907**

**Mtaaluma Mkuu wa Shule 0755238728**

**Shule ya Sekondari Tunduru**
**S.L.P 78**

**Tarehe ………………..**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**S.L.P ……………………………………....**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI TUNDURU HALMASHAURI YA TUNDURU MKOA WA RUVUMA MWAKA …………….**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka………… na atasoma tahasusi ya aliyopangawa OWM-TAMISEMI

Shule ya Sekondari Tunduru inapatikana **Mkoa wa Ruvuma** Wilaya ya **Tunduru.** Shule ipo mjini **TUNDURU** umbali wa kilometa 1.5 kutoka stand kuu ya mabasi ya Tunduru kuelekea upande wa Kaskazini Magharibi. Kokote utokeapo kupitia Dar-es Salaam au Songea unaweza kufika kwa siku moja. Kwa wale watokeao Dar – es -Salaam kuja Tunduru unashauriwa kutumia barabara ya Kilwa kupitia Rufiji, Masasi, Mangaka kisha Tunduru kwa siku moja. Kuna usafiri wa uhakika kwa njia yoyote utakayopita.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe ………….hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe kuanzia tarehe ............ Mwisho wa kuripoti ni tarehe ………..

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. A) Sare ya shule hii ni Suruali mbili za rangi ya light blue **(bluu bahari)** ziwe na mshono wa kawaida, isiyobana, upana wa miguuni usiopungua inchi 18, kwa wenye changamoto ya upatikanaji wa kitaambaa cha suruari huduma ya ushonaji inapatikana maeneo ya shule.

B) Shati nyeupe mbili za mikono mirefu (tetron) zenye kola shingoni siyo za kubana

ii. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi (jozi 2)

iii.Soksi nyeusi jozi mbili au zaidi.

iv).Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali.

v).Sweta la bluu lenye kola ya V (mawili).

vi).Nguo za kushindia Suruali nyeusi mbili zenye vipimo sawa na maelekezo ya kipengele namba (i) hapo juu.

vii).Tisheti (T-shirt) 2 za njano zenye kola.**(Aina ya AIR PILOT/ SPORT)** kwa wenye changamoto ya upatikanaji wa aina hiyo ya T-shirt huduma hiyo inapatikana katika duka la shule.

viii).Tracksuit ya rangi ya light blue **(bluu bahari** kama kitambaa cha suluari).

ix).Nguo za michezo

-SCIENCE- JEZI ZA PSG **RANGI DARK BLUU**

-ARTS - JEZI ZA BAYERN **RANGI NYEKUNDU**

**X) KILA MWANAFUNZI AJE NA PASPORT SIZE 4 ILIYOPIGWA KATIKA KITAMBAA CHA BLUU NYUMA.**

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Daftari (counter book Q3) zisizopungua 12 kwa wanafunzi wote wanaosoma masomo ya sayansi na masomo ya sanaa (arts)

ii. **Ream (A4)** ya Karatasi bunda (2) kwa mwaka;(hutolewa mara moja unaporipoti)

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha imeambatanishwa*);

iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology,(Kwa wenye changamoto ya upatikanaji huduma hii inapatikana katika duka la shule.)

v. Scientific Calculator kwa wanafunzi wote isipokuwa **(wanaosoma HKL)** Kwa wenye changamoto ya upatikanaji kifaa hicho unaweza kuja kununua duka la shule.

vi. Godoro lenye foronya la futi 2½ kwa 6. Kwa wenye changamoto ya upatikanaji kifaa hicho unaweza kuja kununua duka la shule

vii. Mashuka Jozi 3 rangi light blue, blanket 1, mto wa kulalia 1, chandarua 1

viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xi. Kila mwanafunzi aje na trucksuit za lightbluu **(bluu bahari)**
xii. Sanduku la bati na kufuli kwa ajili ya kutunzia vitu awapo shuleni hapa.
xiii. Begi kwa ajili ya kubebea daftari wakati wa kwenda darasani.
xiv. Vifaa vingine kwa mchepuo, Kwanja 1 kwa wanafunzi wote**,** jembe 1 kwa **(HGL,HGK&PCB tu),** Upanga 1 kwa **(PMCs & HGFa tu),** Mopa 1(Squezer) **(wote)** na fagio laini kwa ajili ya ndani**(HKL&PGM tu)** fagio ngumu kwa ajili ya kusugua sakafu**(CBG&PCM tu),** Aidha kila mwanfunzi aje na fagio ya nje (chelewa) **(wote)** Mahitaji haya yaletwe kwa wanafunzi kwa kuangalia mchepuo wake kama ilivyoainishwa
xv. Sabuni ya maji lita 5 **(wote)**kwa mwaka inatolewa unaporipoti.
xvi. Mahitaji mengine kwa ajili ya usafi na afya yake kwa kadri mzazi atakavyoweza
-Sabuni za kufulia (za kutosha) na Sabuni za kuogea (za kutosha)
-Mswaki na dawa ya meno
-Nyembe kwa ajili ya kunyolea ndevu na nywele
-Taulo na Ndala kwa ajili ya kuogea
**-Sandal zitakazovaliwa mara baada ya darasani(sio yeboyebo)**

**2.3 Michango mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

MICHANGO HIYO ILIPWE KATIKA AKAUNT NAMBA **70901100051 JINA TUNDURU SEC.SCHOOL, NMB BANK,** HAKIKISHA UNAANDIKA JINA LA MWANAFUNZI NA UNAWASILISHA BENK SLIP UNAPOKUJA KURIPOTI.
AIDHA KILA MWANAFUNZI UNARIPOTI KATIKA OFISI YA MAKAMU MKUU WA SHULE TUNDURU SEKONDARI.
**ANGALIZO 1.;- HATUPOKEI FEDHA KESHI HIVYO LIPIA BENK KABLA HUJAFIKA KURIPOTI SHULENI, au NENDA DUKA LA SHULE KWA HUDUMA YA KUWEKA BANK KUTUMIA WAKALA KISHA WASILISHA RISITI OFISI YA MAPOKEZI**
**MSISITIZO KILA MWANAFUNZI AWE NA AKAUNT NAMBA AMBAYO ITAMUWEZESHA KUTUNZA FEDHA ZAKE HII ITASAIDIA KUZUIA UPOTEVU WA FEDHA AU KUIBIWA.**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu–TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Night Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi; Atakapohitaji mawasiliano yoyote atatumia simu na namba maalumu kutoka kwa makamu mkuu wa shule bila ya gharama yoyote.(Upekuzi wa mara kwa mara utafanyika).**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

- ❖ **Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani, wakati wa kuja shule anaweza vaa yuniform au nguo hizo za kazi na t-shirt zilizoanishwa hapo juu, shule haitahusika na utunzaji wa nguo zisizotakiwa shuleni.(Upekuzi wa mara kwa mara utafanyika).**

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi wa mali za umma au wanafunzi wenzake
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele,au kunyoa kwa mitindo isiyokubalika Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Kufuga ndevu
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja(ushoga), kuoa au kuolewa.
xi. Kusababisha mimba.
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe ikiwemo kumbi za mipira na nyumba za kulala wageni.
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
xv. Kudharau Bendera ya Taifa.
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu.
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
xviii. Kucheza kamari (betting).

## 4. Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ………………………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule NAMULYA, HAMZA ISMAIL**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**ANGALIZO: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0628160051/0787927992**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0755703438**
- **Mwandamizi Taaluma 0755238728**
- **Mwandamizi Malezi 0765222907**

**FOMU YA KUKUBALI/KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE HII**

**A: KUMBUKUMBU KAMILI:**

1. Jina kamili la mwanafunzi …………………………………………………………………………
2. Taifa ………………………………. tarehe ya kuzaliwa …………………… kabila ……………
3. Mkoa …………………………..….. Wilaya …………………………………… Kata …………
4. Lugha inayozungumzwa nyumbani ………………………… Lugha ya kuzaliwa ……………
5. Jina Kamili la Baba …………………………………………………… Amefariki/Hai …………
6. Jina kamili la Mama…………………………………………………… Amefariki/Hai …………
7. Jina kamili la Mlezi (kama huna wazazi) …………………………………………………………
   Uhusiano wa Mlezi ……………………………………………………………………………
8. Kazi ya Baba/ Mama/ Mlezi ………………………………………………………………………
9. Je umewahi kuwa kiongozi katika shule uliyotoka? NDIYO/ HAPANA ……………………..
10. Michezo unayopenda: (i) …………………………….. (ii) ……………….. (iii) ……………….
11. Sina/Ninayo matatizo ya kiafya kama yapo ni yepi ……………………………………………
12. Andika jina na anuani kamili ya mzazi/mlezi wako inayotumika sasa, pa,moja na namba yake ya simu.
    Jina: ………………………………………………………………………………………….
    Anuani :………………………………………………………………………………………
    Simu: …………………………………………………………………………………………
13. Andika jina na anuani kamili ya ndugu yako wa karibu (kama yupo) ambaye anaishi hapa mjini Tunduru.
    Jina: …………………………………………………………………………………………….
    Anuani: ……………………………………………………………………………………..

**B: KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE HII**

1. **MWANAFUNZI**
   Nimesoma na kuzielewa sheria na taratibu zote za shule na ninakubali/sikubali kujiunga na shule hii. Ninaahidi nitazifuata sheria zote na kuzitekeleza kwa mujibu wa shule inavyotaka na endapo sitofuata taratibu hizo basi nirudishwe nyumbani kwa wazazi
   Jina: ………………………………. Saini: …………………………… Tarehe …………………
2. **MZAZI**
   Nimezisoma sheria, taratibu na kanuni za shule. Nimekaa na mtoto wangu na tumekubaliana kufuata na kutekeleza sheria zote, hivyo hatavunja sheria hizo/kanuni hizo.
   Nimemuasa vya kutosha na amenielewa na endapo itatokea kwenda kinyume na taratibu hizo hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yake.
   Ninakubali kulipa ada na michango yote iliyotolewa na kufuata maelekezo mengine yatakayotolewa na shule. Kijana huyu hana Simu na Sijampatia Simu.

   Jina …………………… Saini: ………Namba ya Simu: …………… Tarehe …………

   Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**……………**
**NAMULYA HAMZA ISMAIL**
**MKUU WA SHULE**

Fomu na. 02

**PMO - RALG**

**RUVUMA REGION:**

**TEL: 0628-160051**

**Tunduru Secondary School,**

**P. O BOX 78**

**TUNDURU**

**REF. NO.** TSS/U/KDT.V/2026

DATE……………………

TO. MEDICAL OFFICER

____________________

____________________

**REF: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

Please, examine Mr. ______________________________Form five ___combination_____As to his fitness for pursuing secondary School studies in this school

**General condition of his Health.**

**Head** Eye/Vision ……………………………………………………………………………………

Ears/Hearing ………………………………………………………………………………

Mouth/Speech ………………………………………………………………………………

Nose ……………………………………………………………………………………………

**Chest X** Ray report:

Blood group ……………………………………………………………………………..…

Stool ……………………………………………………………………………………….

Urine ……………………………………………………………………………………..

HB % ……………………………………………………………………………………………

Leucocytes ………………………………………………………………………………

E.S.R. ……………………………………………………………………………………

Others ……………………………………………………………………………………

**MEDICAL CERTIFICATE:**

I have examined the above named student and consider and recommend him fit/not fit for studies. Special medical recommendation (if any) ……………………………………………………………………

Date ………… Signature ……………………Designation ………………………………………

**TAARIFA ZA NDUGU WATAKAOFIKA KUMUONA NA KUSIKILIZA SHIDA MBALIMBALI ZA MWANAFUNZI**

**JINA LA MWANAFUNZI…………………………KIDATO CHA …...MCHEPUO WA ……………**

**PICHA ZA WAZAZI/WALEZI WAWILI ZIBANDIKWE HAPA**

**A. NDUGU WA KUMTEMBELEA NA KUSIKILIZA SHIDA ZA MWANAFUNZI**

1. **JINA…………………………………JINSIA……… KABILA ……………**
   **ANAKOTOKA………………………UHUSIANO WAKE NA MWANAFUNZI………………………NAMBA YAKE YA SIMU……………………**

2. **JINA…………………………JINSIA……………… KABILA ……………………..**
   **ANAKOTOKA………………UHUSIANO WAKE NA MWANAFUNZI……………….**
   **NAMBA YAKE YA SIMU……………………………………………….**

3. **JINA……………………JINSIA………………… KABILA …………………….**
   **ANAKOTOKA………………………………………………………………..**
   **UHUSIANO WAKE NA MWANAFUNZI…………………………………………….**
   **NAMBA YAKE YA SIMU……………………………………………….**

**B. MZAZI AWAIDHINISHE HAO NDUGU WA MWANAFUNZI.**
**MIMI………………………… MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI…………………………………**
**NINAWAIDHINISHA WATAJWA HAPO JUU KUWA NI NDUGU WA MWANANGU NA WATAKUWA WAKIFIKA KUMUONA NA KUSIKILIZA SHIDA MBALIMBALI WAKATI AMBAO MIMI KAMA MZAZI/MLEZI NITAKUWA NIMESHINDWA KUFIKA.**

**SAHIHI……….. NAMBA YA SIMU ………………………TAREHE…………………………….**

**C. KIONGOZI WA SERIKALI YA MTAA/KIJIJI ATHIBITISHE TAARIFA HII**

**MIMI ……………………….. CHEO …………… KIJIJI/MTAA ……………………………………**
**NATHIBITISHA HAPO JUU WAMETEULIWA NA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI ……………………**
**NA NINAKUOMBA UWAPOKEE WAWE WALEZI MBADALA NA MWANAFUNZI TAJWA APO JUU.**

**SAHIHI ……………… MUHURI ………..… TAREHE …………… NAMBA YA SIMU ……………………….**

Fomu na. 4

## VITABU MUHIMU KWA AJILI YA MASOMO

Ifuatayo ni orodha ya mapendekezo ya vitabu vya ziada ambavyo vinatumika kwaajili ya kujisomea kwa wanafunzi wa kidato cha tano na sita. Ni muhimu sana mzazi/mlezi ukanunua kwaajili ya mwanao walau vitabu viwili kwa kila somo atakalosomea kulingana na mchepuo aliochaguliwa.

**ACADEMIC COMMINICATION (Somo hili linafundishwa kwa wanafunzi wote wa masomo ya sayansi na sanaa)**

1. The ultimate; Academic communicaton advanced level, by Mgonja.

**VITABU KWA MASOMO YA SANAA**

**SOMO LA HISTORY**

1. **Bakari Madaya (2025) History for high schools; form five based on the current syllabus (2023)**
2. **Bakari Madaya (2026) History for high schools; form six based on the current syllabus (2023)**
3. **Idrisa Msuya; learning Advanced History Book 1;Questions and Answer review**
4. **Idrisa Msuya; learning Advanced History Book 2;Questions and Answer review**

**SOMO LA ENGLISH LANGUAGE**

- An Enemy of the people(play) Henrick Ibsen
- Animal farm
- Chasing the leopard finding the lion
- The government inspector
- A taste of heaven
- Summons
- Lament of the silant & other poems
- The opportunist

**SOMO LA GEOGRAPHY**

- Physical Geography by Zisti Kamili
- Physical Geography by Zisti Kamili
- Monkhouse. F. J (1975) Principle of Physical Geography 90, Tottenham Court Road. London: Wip 9he
- Buckle, c (1978). Landforms in Africa. London
- White. R. (1984) physical geography, macmillan, London.

**SOMO LA KISWAHILI**

**(a) Kwa mchepuo wa HGK NA HKL**

- Dunia uwanja wa fujo
- Ua la faraja
- Miradhi ya hatari
- Wasifu wa siti bint saad
- Mukwava wa uhehe

- Shujaa mirambo
- Usaliti mjini
- Fumbo linaoelea
- Malenga wa ziwa kuu
- Andamo msafiri safarini
- Wosia wa baba

**(b) Kwa mchepuo wa HGFa**

- Asali chungu
- Mwana wa yungi hulewa
- Vipuli vya figo
- Kaptula la marx
- Nyerere na safari ya kanani
- Dhifa
- Utenzi majumui wa karne ya 21
- Malenga wa bara

## VITABU KWA MASOMO YA SAYANSI

### SOMO LA PHYSICS

1. S' Chand I (Class Xi)
2. S' Chand II (Class Xii)
3. Nelkon and Parker (Any Edition )
4. Roger and Moncastors
5. Physics review paper 1 2010-2020

### SOMO LA CHEMISTRY

- Chand S. '' Conceptual Chemistry '' Volume XI
- Chand S. '' Conceptual Chemistry '' Volume XII
- Chemistry review paper 1
- Chemistry review paper 2
- Ngaiza, Lusima.(2025) inorganic chemistry with General chemistry. Ngaiza education hub

### SOMO LA BIOLOGY

- Biological science 5$^{th}$ edition by tylor, et al
- Understanding biology by glenn and toole
- Biology review paper 1
- Biology review paper 2
- Chand I (Class Xi)
- Chand II (Class Xii)

### SOMO LA MATHEMATICS

- Pure mathematics I J.K BOOK HOUSE
- Pure mathematics II J.K BOOK HOUSE
- Mathematics review paper 1

- Mathematics review paper 2
- Pure mathematics by C.J TRUNTER
- Advanced mathematics by Chand (class XI)
- Advanced mathematics by Chand (class XII)
- Conceptual Advanced Mathematics for secondary school form v  (petro I. mayombya)
- Conceptual Advanced Mathematics for secondary school form  vi (petro I. mayombya)

**<u>SOMO LA COMPUTER SCIENCE</u>**

1. Tool kit for computer maintenance pc 1.